AUSCO

Programu ya Maelekezo ya Kitamaduni nchini Australia

# Jamii za Waaustralia

Katika Australia kuna aina nyingi mbalimbali za familia na waweze kuwa tofauti sana na aina ya familia unayozoea.

**Familia za Waaustralia zina mchanganyiko mwingi.** Hii ikiwemo ni pamoja na familia za jadi za baba, mama na watoto lakini familia nyingi ina wajumbe wa wazazi kambo na watoto wa kambo; wazazi wa kambo na watoto; ndugu kutunzana; wazazi wa jinsia moja na hata mababu na mabibi kulea wajukuu zao. Inazidi kuwa kawaida kwa familia kuwa familia za mzazi mmoja.

**Familia za Waaustralia zinaweza kuwa na ukubwa wowote.** Familia nyingine zina watoto wawili au kupunguza wakati familia nyingine zinaweza kuwa na watoto watat au wane. Wanawake wengi hupata mtoto wa kwanza wanapokuwa na umri wa miaka thelathini na zaidi na wengine wanachagua kuacha kuwa na watoto wowote.

**Sio Waaustralia wote wanaoishi kama jamii kubwa sana.** Mara nyingi wazazi wakunga wanaweza kuishi peke yao au katika nyumba maalum ambayo wanatunza watu wenye umri mkubwa (mara nyingi huitwa 'nyumba ya kustaafu').

**Wanaume na wanawake wanaweza kuishi pamoja bila kufunga ndoa.** Hii inaitwa uhusiano wa sheria ya kawaida au wa 'de facto' na huu unatambulika kote kijamii na kisheria.

**Waaustralia wapo huru kuoa mtu yeyote kutoka vikundi vya utamaduni tofauti, dini tofauti au rangi tofauti.** Unahitaji kuwa umri zaidi ya 18 kuoana, hata hivyo mahakama yanaweza kupitisha ndoa katika kesi ya maalum kama mmoja wa watu ana umri wa miaka 16 au 17.

**Ndoa za kupangiwa zinakubalika nchini Australia, lakini ndoa za kulazimishwa ni kinyume cha sheria.** Kama watu wote wana nia ya kuoana na wana umri wa zaidi ya miaka 18 wanaweza kuoana. Hakuna mtu anayeweza kulazimishwa kuoa au kuolewa.

**Ni kinyume cha sheria kwa mtu kufunga ndoa na wanaume zaidi wa mmoja au bibi zaidi wa mmoja kwa wakati mmoja.**

**Talaka ni kawaida na inaitikizwa katika jamii.** Ni kawaida kwa watu kufunga ndoa tena baada ya talaka.

**Wanawake wengi Waaustralia hufanya kazi nje mbali na nyumbani.** Wanaume wengi huchukua jukumu kubwa katika kusaidia nyumbani, kwa mfano kwa kufanya manunuzi kwa ajili ya mboga, kupika, kusafisha na kutunza watoto. Katika baadhi ya matukio mwanaume anaweza kukaa nyumbani kutunza watoto na nyumba wakati mwanamke huenda kufanya kazi.

**Vijana barubaru mara nyingi hupata ajira ya wakati mfupi ili kupata pesa na kujifunza ustadi upya.** Hii hutoa kwao uzoefu wa thamani pamoja na nafasi ya kupata fedha kwa ajili yao wenyewe na kama ni lazima, ili kusaidia kulipa bili ya kaya ya familia.






Ukurasa huu umewachwa tupu makusudi

Australian Government
Department of Social Services

Inaletwa kwako na Shirika la Uhamiaji la Kimataifa kwa niaba ya Idara ya Huduma za Jamii nchini Australia

IOM • OIM